




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 21. Msimu wa Kilimo 2019/20


Tathmini Aprili 21-30, 2020 na Matazamio kwa Kipindi cha Mei 1-10, 2020

MUHTASARI

- Unyevunyevu wa udongo uliokithiri unaweza kuathiri ukuaji wa mazao pamoja na uharibifu wa baadhi ya mazao
- Hali ya unyevunyevu katika hewa na udongo vinaweza kuchangia kuenea kwa wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea
- Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya ushauri huu.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii ilisababisha kusukumwa kwa ukanda wa mvua kuelekea kaskazini mwa nchi. Uwepo wa Joto la bahari la juu wa wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi ulisababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la chini wa wastani, hali iliyopelekea kuwa na mchango mkubwa katika kuleta upepo wenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Congo kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi. Kwa ujumla, uwepo wa migandamizo midogo ya hewa, joto la chini kidogo ya wastani kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki pamoja na kuimarika kwa wimbi anga ("Madden Julian Oscillation, MJO") kulikua na mchango mkubwa wa kutokea kwa mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 21-30, 2020

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020

Maeneo mengi ya magharibi, ukanda wa Ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani yamepata mvua kati ya mm 50 hadi mm 200. Kiasi cha mvua cha zaidi ya mm 200 kimerekodiwa katika mkoa wa Mara pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, upungufu wa mvua umeonekana katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua ambapo kiasi cha chini ya mm 26 kilipimwa katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Iringa, Mtwara na maeneo ya kusini mwa mikoa ya Morogoro na Lindi kama inavyoonekana katika Kielelezo.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020

Katika kipindi cha dekadhi iliyopita, mazao yameendelea vizuri kutokana na mvua za msimu zinazoendelea. Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa. Wakulima katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Njombe, Mbeya, Rukwa, Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma waliendelea na shughuli za uvunaji wa maharagwe na mahindi, ingawaje athari za fangasi zimeonekana kwenye maharagwe katika baadhi ya maeneo mengi kutokana na unyevunyevu uliokithiri kwenye udongo. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Kagera, Morogoro na

Arusha mahindi yapo katika hatua ya kukomaa, pia wakulima waliendelea na shughuli za upulizaji wa dawa za kuuwa wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Maeneo machache ya mkoa wa Mara yameripoti kuwepo kwa viwavi jeshi vamizi. Vilevile, katika mkoa wa Kagera maharagwe yameharibiwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha. Mafuriko yaliyoripotiwa katika mkoa wa Kilimanjaro yameleta athari ya mumomonyoka wa udongo na kutuama maji mashambani. Aidha, maeneo machache ya ukanda wa pwani wa kaskazini (Morogoro, Tanga, na visiwa vya Pemba, na Unguja) zao la mpunga lilikuwa katika hatua ya kukomaa pamoja na kuwepo hali ya kutuama kwa maji mengi mashambani.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan katika mabonde ya ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, Rukwa, Ruvuma, Rufiji na Nyasa kutokana na mvua zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2020.

Mifumo ya migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuongezeka nguvu. Hali hii itaendelea kuusukuma ukanda wa mvua kaskazini zaidi mwa nchi. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na joto la chini ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki, karibu na pwani ya Angola. Hali hii inatarajiwa kusababisha vipindi vya migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuimarisha upepo kuvuma kutoka magharibi hususan misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya nchi. Vilevile, hali hii inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi mwa nchi, ukanda wa Ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2020.

Maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) kunatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo, hususan magharibi na mashariki mwa ziwa Viktoria. Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha,

Manyara na Kilimanjaro) na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo, hususan katika nusu ya pili ya dekad. Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika maeneo machache. Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache. Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) kunatarajiwa kupata mvua nyepesi hususan kipindi cha nusu ya pili ya dekad.

HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2020

Hali ya unyevunyevu katika udongo inatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hali ambayo itasaidia ukuaji wa mazao. Hata hivyo hali ya unyevunyevu uliokithiri hususan katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kagera na Kilimanjaro umesababisha Fangasi kuathiri mazao hivyo wakulima wanashauriwa kuendelea kutumia dawa za kuzuia wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Katika maeneo machache ya mkoa wa Mara ambako kumeripotiwa uwepo wa viwavi jeshi vamizi wakulima wanashauriwa kuendelea na upulizaji wa madawa ya kuulia wadudu waharibifu wa mazao. Hali ya unyevunyevu katika udongo na malisho kwa wanyama vinatarajiwa kuwa vya kutosha katika maeneo mengi ya nchi. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya ushauri huu.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2020

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya mifereji ya umwagiliaji na mabwawa, piakuchukua tahadhari juu ya majanga yaletwayo na mafuriko.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania